

TANGAZO



BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR

MUONGOZO WA USAJILI NA UHAKIKI WA WATAHINIWA WA KIDATO CHA PILI, DARASA LA SABA NA NNE KATIKA MITIHANI YA TAIFA KWA MWAKA 2022.

Baraza la Mitihani la Zanzibar linawatangazia kuwa usajili wa watahiniwa katika Mitihani ya Taifa wa Darasa la Nne (4), Saba (7) na Kidato cha Pili umeanza kuanzia tarehe 18/04/2022 na kumalizika ifikapo tarehe 17/07/2022, hivyo walimu wakuu na wasajili wanatakiwa kuendelea kujaza taarifa za wanafunzi kwa usahihi na kiukamilifu kupitia Mfumo wa Usajili " **OZEMS**"

USAJILI WA WATAHINIWA

Usajili mpya utafanyika kwa watahiniwa wa Darasa la Nne tu, kwa upande wa darasa la Saba na kidato cha Pili taarifa zao za awali tayari zimeshasajiliwa katika Mfumo wa "OZEMS", hatua inayofuatia ni kupandihisa majina ya watahiniwa waliopo sasa katika skuli husika.

MAMBO YA KUZINGATIA KATIKA USAJILI WA MITIHANI YA TAIFA

Majina ya watahiniwa yaandikwe kikamilifu (majina matatu (3) na yatokane na cheti cha kuzaliwa)

Taarifa zinazohusiana na usajili wa watahiniwa zijazwe kikamilifu kama ilivyoelekezwa katika fomu ya usajili.

MASHARTI YA USAJILI WA WANAFUNZI WA DARASA LA SABA NA KIDATO CHA PILI

Ili Mtahiniwa aweze kusajiliwa katika mfumo ni lazima awe na sifa zifuatazo:-

- Kwa watahiniwa wa Darasa la Saba awe amefanya Mtihani wa Darasa la Nne na kufaulu.
- Kwa watahiniwa wa kidato cha Pili awe amefanya Mtihani wa Darasa la Sita na kufaulu
- Aidha wanafunzi waliofeli mtihani wa Taifa watatakiwa kurudia mtihani mwaka 2022
- Mtahiniwa asajiliwe katika masomo yasiyopunguwa Nane (8) na yasiyozidi Kumi na Mbili (12) kwa Kidato cha Pili.
- Kwa Wanafunzi waliosoma nje ya Zanzibar watatakiwa kuwasilisha **Baraza la Mitihani la Zanzibar** uthibitisho wa kukubaliwa kusoma katika Skuli za Zanzibar kutoka kwa **Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali** ikiambatanishwa na matokeo ya mtihani ya mtahiniwa.
- Utaratibu wa uchaguzi wa masomo ni lazima uendane na Mtaala.
- Tarehe ya kuzaliwa pamoja na jinsi ya mtahiniwa viandikwe kwa usahihi.

NB: WATAHINIWA AMBAO MAJINA YAO HAYALINGANI NA MADARASA YALIYOPITA

Kwa Watahiniwa ambao Majina yao hayalingani baina ya cheti cha kuzaliwa na kwenye Mfumo, Msajili atahitajika kujaza taarifa za mtahiniwa huyo kwenye fomu maalumu na kuambatanisha Nakala ya cheti cha kuzaliwa cha mtahiniwa husika na kuiwasilisha kwa Afisa Elimu Wilaya, kwa muda usiozidi Tarehe **20-05-2022**

WATAHINIWA WENYE MAHITAJI MAALUM

Wanafunzi wenye Ulemavu wabainishwe aina za ulemavu katika mfumo kwa kuweka alama sahihi inayotumika ambazo ni Asiyeona (Blind-BR), Mwenye Uoni hafifu (Low Vision-LV), Mwenye matatizo ya kuskia (Hearing Impairment-HI), wenye mtindio wa ubongo (Intellectual Impairment-II) au Ulemavu mwengine wa viungo (Physical Impairment-PI).

Watahiniwa ambao watakuwa wana mahitaji mengine (Other) watalazimika kuandika barua kuelezea aina ya ulemavu huo.

UTARATIBU WA MALIPO

Skuli za Binafsi zinatakiwa kulipia ada ya usajili wa Mitihani ya Taifa kwa kutumia **Control Number** ambayo inatolewa na Ofisi ya Muhasibu wa Baraza la Mitihani la Zanzibar.



FOMU YA MAREKEBISHO YA MAJINA YA WATAHINIWA 2022

JINA LA SKULI..... DARASA / KIDATO.....

SN	JINA KAMILI LILILOTAHINIWA	NAMBA YA MTIHANI	MWAKA	JINA SAHIHI (CHETI CHA KUZALIWA)

SN	JINA KAMILI LILILOTAHINIWA	NAMBA YA MTIHANI	MWAKA	JINA SAHIHI (CHETI CHA KUZALIWA)

JINA LA MSAJILI..... SAINI..... TAREHE.....

TANBIHI: TAFADHALI AMBATANISHA KIVULI CHA CHETI CHA KUZALIWA CHA MTAHINIWA HUSIKA

Baraza la Mitihani la Zanzibar, Vuga Zanzibar - Tanzania, S.L.P 3070,
Tovuti: www.bmz.go.tz, email: info@bmz.go.tz